# Ujinsishaji wa Mwanaume katika Nyimbo za Bongo Fleva: Uwakilishi wa Uanaume, Utamaduni na Nguvu za Kijamii

**Lilian K. Kaishozi**

*Chuo Kikuu cha St John's cha Tanzania, Dodoma*

lkaishozi@yahoo.com

&

**Felistas R. Mahonge**

*Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DarTU), Dar es Salaam*

*felistas.mahonge@dartu.ac.tz*

**Ikisiri**

*Makala hii inachunguza ujinsishaji wa mwanaume katika nyimbo za Bongo Fleva kupitia uwakilishi wa uanaume, mahusiano ya kijinsia, majukumu ya kijamii, uchumi, mapenzi na uanaume mseto unaojengwa na mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na nguvu za kijamii. Utafiti uliongozwa na malengo matatu: kuchunguza namna uwasilishaji wa uanaume, mahusiano ya kijinsia na majukumu ya kijamii vinavyojenga ujinsishaji wa mwanaume katika nyimbo za Bongo Fleva; kuchambua namna uchumi, mapenzi na migogoro ya mahusiano vinavyojitokeza katika ujinsishaji na uwakilishi wa uanaume; na kuchunguza namna uanaume mseto unavyojengwa kupitia mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na nguvu za kijamii katika nyimbo za Bongo Fleva. Aidha, utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uanaume Hegemonia ya Connell na Messerschmid, Nadharia ya Utendaji wa Jinsia ya Butler, Nadharia ya Uwakilishi ya Hall pamoja na Nadharia ya Mseto wa Utamaduni ya Bhabha. Mkabala wa kimaelezo ulitumika pamoja na uchambuzi wa kimaudhui katika kuchambua nyimbo kumi za Bongo Fleva zilizochaguliwa kwa usampulishaji lengwa kutokana na uwezo wake wa kuwakilisha maudhui ya uanaume, mahusiano, mamlaka na changamoto za kijamii. Data za msingi zilipatikana kupitia usikilizaji wa nyimbo, uchambuzi wa mashairi na video za muziki kutoka majukwaa ya kidijitali, huku data za upili zikitokana na vitabu, makala za kitaaluma na nyaraka za maktaba. Matokeo yanaonesha kuwa mwanaume katika Bongo Fleva huwasilishwa kama mhimili wa familia, mtoa huduma na mwenye mamlaka, lakini pia kama mhanga wa maumivu ya kihisia, usaliti na shinikizo la kiuchumi na kijamii. Hivyo, muziki huu hujenga uanaume wa kimseto unaochanganya maadili ya ndani na ushawishi wa kimataifa. Makala hii inachangia mjadala wa jinsia na utamaduni kwa kuonesha kuwa uanaume ni eneo la mivutano, mabadiliko na ujenzi unaoendelea katika jamii ya kisasa.*

**Istilahi Muhimu**: *ujinsiishaji, uanaume, uwakilishi, utamaduni, na nguvu za kijamii*

**Utangulizi**

Kwa miongo mingi, tafiti na mijadala kuhusu jinsia zimejikita zaidi katika kuchunguza changamoto zinazowakabili wanawake, huku uzoefu wa wanaume ukibaki pembezoni mwa tafiti za kitaaluma. Wanaharakati, watafiti na wasanii wameelekeza nguvu kubwa katika kufichua ukandamizaji na ubaguzi dhidi ya wanawake, hatua iliyochangia maendeleo muhimu katika usawa wa kijinsia. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, tafiti za uanaume zimeanza kubainisha kuwa mwanaume naye huathiriwa na mifumo ya kijamii inayomjengea matarajio magumu kuhusu nguvu, mamlaka na uthabiti wa kihisia.

Katika muktadha huo, dhana ya ujinsishaji (*engendering*) imeelezwa kama mchakato wa kubainisha, kuchambua na kuondoa ubaguzi na ukandamizaji unaotokana na mifumo ya kijinsia (Mlaga, 2017). Katika utafiti huu, ujinsishaji wa mwanaume unahusu kufichua na kuchunguza changamoto zinazotokana na matarajio ya kijamii kama vile ulazima wa mwanaume kuonekana imara daima, ukandamizaji wa kihisia, lugha potofu kuhusu uanaume, pamoja na unyanyasaji na shinikizo za kiuchumi na kijamii. Dhana hii inahusishwa pia na harakati za kukuza usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali za maisha ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni (Rao, 2014; Caywood & Darmstadt, 2024; Talakinu, 2023; John & Kilatu, 2025).

Katika fasihi na tafiti za Kiafrika, mwanaume mara nyingi amewakilishwa kama mhimili wa mfumo dume, mlinzi wa familia au mnyanyasaji, huku uzoefu wake wa kihisia na changamoto zake za kijamii zikipewa uzito mdogo (Adichie, 2013; Lawson, Dubin & Mwambene, 2019; 2020). Ingawa tafiti za hivi karibuni zimeanza kuangazia nafasi ya mwanaume katika muktadha wa Kiafrika (Bjarnesen et al., 2023; Babalola, 2023; Mwakibete, 2022), bado kuna pengo kubwa la kitaaluma katika kuelewa kwa kina jinsi uanaume unavyojengwa, kuwakilishwa na kupingwa katika sanaa maarufu.

Nyimbo za Bongo Fleva zinatoa jukwaa muhimu la kuchunguza mchakato huu wa kijamii na kitamaduni. Kama aina ya muziki wa kisasa unaochanganya mitindo ya kimataifa na tamaduni za ndani kupitia lugha ya Kiswahili (Perullo, 2011; Suriano, 2021), Bongo Fleva si burudani tu bali ni chombo cha uzalishaji wa maana za kijinsia na kijamii. Kupitia nyimbo hizo, uanaume huwasilishwa kama nguvu ya mamlaka, mafanikio na uthabiti, lakini pia kama eneo la migogoro

ya kihisia, shinikizo la kiuchumi na mapambano ya utambulisho (Connell & Messerschmidt, 2005; Kimmel, 2017).

Kwa kutumia nadharia za uanaume hegemonia ya Connell na Messerschmidt (2005), utendaji wa kijinsia ya Butler (1990), pamoja na uwakilishi wa Hall (1997), utafiti huu unaeleza kuwa uanaume si hali ya kiasili bali ni ujenzi wa kijamii unaorudiwa kupitia lugha, utamaduni na mawasiliano ya kijamii. Aidha, mseto wa kitamaduni wa Bhabha (1994) unaonesha jinsi athari za utandawazi na tamaduni za ndani zinavyozalisha uanaume wa kisasa wenye mivutano na mabadiliko endelevu.

Kwa ujumla, utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza ujinsishaji wa mwanaume katika nyimbo za Bongo Fleva kwa kuchambua uwakilishi wa uanaume, utamaduni na mivutano ya nguvu za kijamii. Kupitia uchambuzi wa kina wa nyimbo teule, utafiti unatarajia kuchangia katika mjadala wa taaluma za jinsia na utamaduni kwa kuonesha kuwa uanaume ni ujenzi wa kijamii unaobadilika, unaogongana na unaojadiliwa katika nyanja za kisasa za muziki na maisha ya kila siku.

## Lengo la Utafiti

Kuchunguza ujinsishaji wa mwanaume katika nyimbo za Bongo Fleva kupitia uwakilishi wa uanaume, mahusiano ya kijinsia, majukumu ya kijamii, uchumi, mapenzi na uanaume mseto unaojengwa na mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na nguvu za kijamii. Kwa umahususi, utafiti umeazimia:

1) Kuchunguza namna uwasilishaji wa uanaume, mahusiano ya kijinsia na majukumu ya kijamii vinavyojenga ujinsishaji wa mwanaume katika nyimbo za Bongo Fleva.
2) Kuchambua namna uchumi, mapenzi na migogoro ya mahusiano vinavyojitokeza katika ujinsishaji na uwakilishi wa uanaume ndani ya nyimbo za Bongo Fleva.
3) Kuchunguza namna uanaume mseto unavyojengwa kupitia mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na nguvu za kijamii katika nyimbo za Bongo Fleva.

## Mapitio ya Maandiko Kuhusu Ujinsiishaji na Nyimbo za Bongo Fleva

### *Ujinsishaji wa Jinsia katika Fasihi, Muziki na Mijadala ya Kijinsia*

Mapitio haya yanachambua maandiko kuhusu ujinsishaji *(engendering*) kwa kuonesha kuwa tafiti nyingi zimejikita zaidi katika nafasi na changamoto za mwanamke, huku sauti ya mwanaume ikibaki pembezoni. Kwa ujumla, fasihi ya kijinsia imeonesha kuwa mahusiano ya kijamii huzalishwa ndani ya mifumo ya nguvu isiyo sawa kati ya wanawake na wanaume; hata hivyo, mkazo mkubwa umewekwa katika mwanamke kama mhanga wa mfumo dume kuliko kuchunguza namna mwanaume naye anavyoundwa na kushinikizwa na matarajio ya uanaume. Kwa mfano, Struwig na Roberts (2014) katika *Engendering Change: Attitudes towards Women in Politics in South Africa* wanasisitiza umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika siasa na uwakilishi wa kijinsia, lakini wanaacha pengo kuhusu athari za mifumo hiyo kwa wanaume. Vivyo hivyo, Our Watch (2018) katika *Challenging Gender Stereotypes in the Early Years* wanaonesha namna familia na vyombo vya habari vinavyojenga mitazamo ya kijinsia tangu utotoni, ingawa shinikizo la ujenzi wa uanaume halijachambuliwa kwa kina. Aidha, Dubin na Mwambene (2019) katika *Ensuring African Women's Access to Justice* wanaeleza changamoto za wanawake katika upatikanaji wa haki, huku nafasi ya mwanaume katika shinikizo la kiuchumi ikibaki hafifu.

Kwa upande wa tafiti za uanaume, Bjarnesen na wenzake (2023) wanaonesha kuwa mabadiliko ya kiuchumi na utandawazi yamebadilisha namna wanaume wa Afrika wanavyojitambulisha na kutekeleza majukumu yao, jambo linalothibitisha uanaume kama ujenzi wa kijamii unaobadilika. Aidha, Babalola (2023) anaeleza kuwa muziki wa *Hip Hop* na *Afrobeats* ni jukwaa la kujadili utambulisho wa kijinsia, ingawa uchambuzi wa mwanaume kama mhanga wa kihisia bado ni mdogo. Hivyo, maandiko haya yanaweka msingi muhimu wa uelewa wa ujinsishaji, lakini pia yanaonesha pengo la kiutafiti kuhusu uanaume kama mfumo unaobeba shinikizo za kijamii, kiuchumi na kihisia—pengo ambalo utafiti huu unalenga kuliziba kupitia uchambuzi wa Bongo Fleva.

### *Uwakilishi wa Jinsia na Ujinsishaji wa Mwanaume katika Nyimbo za Bongo Fleva na Fasihi*

Bongo Fleva ni chombo muhimu cha kuakisi maisha ya jamii ya Tanzania, kikijadili siasa, uchumi, mapenzi, utandawazi na mahusiano ya kijinsia. Tangu kuibuka kwake miaka ya 1990, muziki huu

umetumika kama jukwaa la kuwasilisha nguvu za kijamii na matarajio ya vijana. Perullo (2005) na Suriano (2007) wanaeleza kuwa uliibuka kama sauti ya vijana wa mijini wanaokabiliwa na changamoto za kiuchumi, ukosefu wa ajira na mabadiliko ya utandawazi, hali inayodhihirisha namna muziki huu unavyoakisi mivutano ya kijamii kati ya ndoto na uhalisia wa maisha.

Katika muktadha wa utafiti huu, hali hiyo inaonesha kuwa Bongo Fleva si burudani tu bali pia ni eneo muhimu la kujenga na kuwasilisha ujinsishaji wa mwanaume. Kupitia mazingira ya kiuchumi na kijamii yanayoelezwa na Perullo (2005) na Suriano (2007), mwanaume huwasilishwa kama mhusika anayekabiliwa na shinikizo la mafanikio, uthibitisho wa kiuchumi na matarajio ya kijamii. Hivyo, muziki huu unakuwa kioo cha namna uanaume unavyojengwa, kujaribiwa na wakati mwingine kubadilishwa ndani ya muktadha wa mabadiliko ya kijamii ya Tanzania ya kisasa.

Tafiti za kijinsia zimeonekana kujikita zaidi katika ujinsiishaji wa mwanamke, lakini maendeleo ya hivi karibuni yanaonesha kuwa mwanaume pia huathiriwa na mifumo ya kijamii na kiutamaduni. Mulvey (1975) kupitia *male gaze* anaeleza jinsi vyombo vya sanaa humuweka mwanamke kama kitu cha kutazamwa, ingawa Gill (2009) anaonesha kuwa hata mwanaume huwekwa chini ya tathmini ya mwili, nguvu na mafanikio kama bidhaa ya kijamii. Vilevile, Connell (1995) na Nnaemeka (1998) wanaeleza kuwa mfumo wa kijinsia huweka mashinikizo kwa wanaume yanayosababisha maumivu ya kihisia na kijamii, ambapo mwanaume huwasilishwa kama mwenye uimara wa kudumu huku udhaifu wake ukifichwa. Khamis (2020) anaonesha kuwa baadhi ya nyimbo huendeleza mfumo dume kwa kumwonesha mwanaume kama mwenye mamlaka ya kifedha na mwanamke kama mtegemezi, ingawa tafiti za hivi karibuni zinaonesha mabadiliko ambapo wanawake hupewa nafasi za nguvu za kiuchumi

Katika muktadha wa Tanzania, tafiti bado ni chache, ingawa baadhi ya nyimbo za Bongo Fleva zinaanza kumwonesha mwanaume kama mhanga wa mahusiano, umasikini na shinikizo la kijamii. Kwa mfano, John na Kilatu (2025) wanaonesha mabadiliko ya nafasi za kijinsia ambapo mwanaume anaweza kuwa mtegemezi wa kihisia au kifedha. Hivyo, kuna pengo la kiutafiti kuhusu ujinsiishaji wa mwanaume katika muziki wa Tanzania, hasa kupitia lugha, taswira na maudhui ya Bongo Fleva.

***Dhana ya Uanaume na Uanaume Hatarishi katika Jamii ya Kisasa***

Tafiti zinaonesha kuwa uanaume si hali ya kibaiolojia bali ni ujenzi wa kijamii unaojumuisha matarajio ya nguvu, mamlaka na uwajibikaji wa kifedha. *Connell* (1995) kupitia dhana ya uanaume tawala (*hegemonic masculinity*) anaeleza kuwa jamii huweka viwango vinavyomlazimisha mwanaume kuwa jasiri, mwenye mamlaka na asiyeonesha udhaifu wa kihisia. Aidha, *Silberschmidt* (2001) anaonesha kuwa mabadiliko ya kiuchumi yamepunguza nafasi ya mwanaume kama mtegemezi mkuu wa familia, hivyo kuchochea migogoro ya kijinsia na msongo wa mawazo.

Vivyo hivyo, *Ratele* (2013) na *Mhando* (2020) wanaeleza kuwa shinikizo la kuthibitisha uanaume kupitia mafanikio ya kifedha na mamlaka katika mahusiano husababisha baadhi ya wanaume kutumia tabia za ukali au kuficha hisia zao. Katika muktadha mpana, Kupers (2005) anaeleza uanaume hatarishi (*toxic masculinity*) kama mfumo unaowasukuma wanaume kuthibitisha uanaume wao kupitia ubabe, ushindani na ukandamizaji wa hisia.

Hivyo, tafiti hizi kwa pamoja zinaonesha kuwa uanaume ni ujenzi unaobadilika na wenye migogoro, lakini bado hazijachunguza kwa kina namna ujenzi huo unavyowakilishwa katika Bongo Fleva. Kwa msingi huo, utafiti huu unachunguza jinsi muziki huo unavyojenga, kuendeleza au kupinga uanaume na uanaume hatarishi katika jamii ya Tanzania.

***Pengo la Kiutafiti na Mwelekeo wa Utafiti***

Pamoja na mchango wa tafiti hizo, bado kuna pengo la kiutafiti kuhusu namna Bongo Fleva inavyowakilisha wanaume kama wahanga wa nguvu za kijamii, kiuchumi na kihisia. Tafiti nyingi zimejikita zaidi katika wanawake na mfumo dume, huku zikitoa nafasi ndogo kwa uchambuzi wa ujenzi wa uanaume ndani ya mabadiliko ya kijamii. Aidha, matumizi ya lugha ya picha, taswira na tamathali za semi katika kujenga maana za uanaume hayajachunguzwa kwa kina.

Kutokana na pengo hilo, utafiti huu unalenga kuchunguza namna nyimbo za Bongo Fleva zinavyomjenga mwanaume kama mhusika anayepitia shinikizo la uanaume, maumivu ya kihisia na matarajio ya kijamii, ili kuelewa namna muziki unavyoakisi mabadiliko ya kijamii na migogoro ya kijinsia katika jamii ya Tanzania ya sasa.

## Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia nne ambazo ni Nadharia ya Uanaume Hegemonia ya R. W. Connell na James W. Messerschmidt (2005), Nadharia ya Utendaji wa Jinsia ya Judith Butler (1990), Nadharia ya Uwakilishi ya Stuart Hall (1997), pamoja na Nadharia ya Mseto wa Utamaduni ya Homi K. Bhabha (1994). Kwa pamoja, nadharia hizi zinaonesha kuwa uanaume katika muziki wa Bongo Fleva si hali ya asili au utambulisho thabiti, bali ni ujenzi wa kijamii na kitamaduni unaozalishwa kupitia lugha, taswira, maudhui na nguvu za kijamii.

Katika lengo la kwanza, Nadharia ya Uwakilishi ya Hall (1997) itatumika kuchunguza namna nyimbo za Bongo Fleva zinavyomwasilisha mwanaume kupitia taswira za nguvu, mamlaka, mapenzi na majukumu ya kijamii, na hivyo kuchangia katika ujinsishaji wake ndani ya matini za muziki. Kwa lengo la pili, Nadharia ya Uanaume tawala/Hegemonia ya Connell na Messerschmidt (2005) pamoja na Nadharia ya Utendaji wa Jinsia ya Butler (1990) zitatumika kuchambua namna uchumi, mapenzi na migogoro ya mahusiano vinavyojitokeza kama maeneo ya kuthibitisha na kuigiza uanaume kupitia matendo yanayojirudia katika lugha, mashairi na taswira za muziki.

Aidha, katika lengo la tatu, Nadharia ya Mseto wa Utamaduni ya Bhabha (1994) itasaidia kueleza jinsi uanaume mseto unavyojengwa kupitia mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na nguvu za kijamii ndani ya Bongo Fleva. Kwa ujumla, kiunzi hiki cha nadharia kinaonesha kuwa uanaume katika Bongo Fleva ni zao la michakato ya kijamii, kitamaduni na kisanaa inayohusisha uwakilishi, utendaji wa kijinsia, mamlaka na mabadiliko ya kitamaduni katika jamii ya Tanzania ya kisasa.

Kwa ujumla, kiunzi hiki cha nadharia kinaonesha kuwa uanaume katika Bongo Fleva ni zao la michakato ya kijamii, kitamaduni na kisanaa inayohusisha uwakilishi, utendaji wa kijinsia, mamlaka na mwingiliano wa tamaduni. Hivyo, nadharia hizi zitasaidiana katika kuchambua namna muziki wa Bongo Fleva unavyomjenga, kumwasilisha na kumjinsisha mwanaume katika jamii ya kisasa ya Tanzania.

## Methodolojia

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo ili kuchunguza maana, lugha na taswira za kijamii zinazojengwa kupitia nyimbo za Bongo Fleva kama kazi za sanaa. Muundo wa utafiti ulikuwa uchambuzi wa maudhui, ambapo nyimbo zilichukuliwa kama matini za kitamaduni zinazobeba maana za kijamii na kijinsia. Eneo la utafiti lilikuwa muziki wa Bongo Fleva nchini Tanzania, huku sampuli ikijumuisha nyimbo kumi (10) zilizochaguliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa kutokana na uhusiano wake na mada ya uanaume na ujinsishaji.

Data ziligawanyika katika data za awali na data za upili. Data za awali zilipatikana kupitia usikilizaji wa nyimbo, uchambuzi wa audio/video na usomaji wa mashairi ya nyimbo teule. Data za upili zilijumuisha vitabu, makala za kitaaluma, tafiti za awali na vyanzo vya mtandaoni kuhusu jinsia, muziki na utamaduni. Ukusanyaji wa data ulifanyika kupitia usikilizaji wa kina na usomaji wa matini, huku uchambuzi wa data ukitumia uchambuzi wa maudhui wa kimaudhui ili kubaini mifumo ya maana inayojitokeza katika nyimbo. Ili kuongeza uhalali wa matokeo, utafiti ulitumia triangulation kwa kulinganisha vyanzo, nadharia na matini mbalimbali. Aidha, maadili ya utafiti yalizingatiwa kwa kuheshimu haki miliki za wasanii na kutumia nyimbo kwa madhumuni ya kitaaluma pekee.

## Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti na Mjadala

### *Uwasilishaji wa Uanaume, Mahusiano ya Kijinsia na Majukumu ya Kijamii*

Sehemu hii inachunguza namna nyimbo za Bongo Fleva zinavyomwakilisha mwanaume kupitia taswira mbalimbali za uanaume, mahusiano ya kijinsia na majukumu ya kijamii. Kwa kutumia Nadharia ya Uwakilishi ya Hall (1997), uchambuzi unaonesha kuwa uanaume si ukweli wa asili bali ni ujenzi wa kiutamaduni unaozalishwa kupitia lugha, taswira na ishara zinazorudiwa katika nyimbo. Hivyo, maana ya "*kuwa mwanaume*" hujengwa kupitia mifumo ya uwakilishi inayomwonesha mwanaume kama mtoa riziki, mwenye mamlaka, mpenzi, au mhanga wa changamoto za kijamii na kihisia.

Katika "*Mume Bwege*" ya Bushoke, uanaume unajengwa kupitia uwezo wa kifedha na utimilifu wa wajibu wa kifamilia. Neno "*bwege*," linalobeba maana ya upungufu wa uwezo na maamuzi, linatumika kama chombo cha kumvua mwanaume hadhi ya kijinsia pale anaposhindwa kuwa mtoa huduma. Kauli kama "*huna hata hela ya nyumbani*" zinaonesha kuwa thamani ya mwanaume

inapimwa kupitia uwezo wake wa kiuchumi. Hapa kushindwa kifedha kunatafsiriwa kama kushindwa kuwa mwanaume. Mtazamo huu unaendana na Silberschmidt (2001), anayeeleza kuwa mabadiliko ya kiuchumi katika Afrika Mashariki yamezalisha mgogoro wa uanaume kwa wanaume wanaoshindwa kutimiza jukumu lao la utoaji huduma kwa familia. Vivyo hivyo, Hooks (2004) anaonesha kuwa mfumo dume huwafundisha wanaume kuthibitisha uanaume wao kupitia mamlaka na uwezo wa kiuchumi, hali inayogeuza mafanikio ya kifedha kuwa kipimo cha thamani ya mwanaume.

Kwa upande wa "*Zali la Mentali*" ya Prof. Jay, uanaume unajengwa kama hali ya mapambano yasiyo na uhakika ndani ya maisha ya mjini. Kauli kama "*zali la mentali linacheza na maisha*" na "*maisha ya mjini ni kujipanga*" zinaonesha mwanaume anayepambana kuhalalisha uwepo wake katika mazingira ya ushindani na ukosefu wa uhakika wa kiuchumi. Hapa uanaume unakuwa mchakato endelevu wa kujithibitisha binafsi mbele ya changamoto za umasikini, ukosefu wa ajira na shinikizo la kijamii. Kimmel (2020) anaeleza kuwa uanaume wa kisasa huingia katika mgogoro pale matarajio ya mafanikio yanapokutana na uhalisia wa kushindwa kuyafikia, jambo linalomlazimisha mwanaume kuendelea kuthibitisha uwezo wake bila kikomo.

Katika "*Ndio Mzee*," Profesa Jay anauwasilisha uanaume kama matokeo ya uthibitisho wa kijamii. Kauli "*ndio mzee*" inafanya kazi kama ishara ya kukubalika ndani ya jamii ya wanaume, ambapo hadhi ya kijinsia hutegemea ridhaa ya wengine. Hii inaonesha kuwa mwanaume "kamili" si yule mwenye sifa za asili bali anayekubalika kijamii kupitia lugha na mawasiliano ya kila siku. Kwa mujibu wa Hall (1997), utambulisho hujengwa kupitia mifumo ya uwakilishi ambapo lugha hurudiwa na kuhalalishwa kama ukweli wa kijamii. Hivyo, uanaume hapa unaonekana kama matokeo ya mazungumzo ya kijamii yanayohitaji uthibitisho wa mara kwa mara.

Hata hivyo, nyimbo za Bongo Fleva pia zinaonesha mabadiliko ya uanaume kuelekea eneo la hisia, starehe na mvuto wa kimapenzi. Katika "*Bora Ni Enjoy*" ya Diamond Platnumz Pamoja na Jux, mwanaume hachorwi tena kama mhusika anayevumilia mateso kimya kimya, bali kama anayepaswa kuonekana mwenye furaha, "*swag*" na maisha mazuri mbele ya jamii. Kauli kama "*bora ni enjoy maisha mafupi ni simple*," "*ya nini niteseke roho*," na "*stress siwezi*" zinaonesha uanaume unaojengwa kupitia starehe na anasa. Kwa mujibu wa Butler (1990), uwakilishi huu unaundwa na utendaji wa kijinsia (*gender performativity)* ambapo mwanaume hujenga utambulisho wake kupitia vitendo vinavyorudiwarudiwa kama kuonesha mafanikio, kujiamini na

kushiriki maisha ya anasa hadharani. Hata hivyo, starehe hiyo pia inaficha uchovu wa kihisia, kwani kauli kama "*ya nini niteseke roho*" zinaashiria jitihada za kukimbia msongo wa maisha kupitia starehe. Ratele (2013; 2020) na Morrell na wenzake (2020) wanaonesha kuwa wanaume wengi wa Afrika na hasa wale wa mjini hutumia maonesho ya maisha ya kifahari kama njia ya kukabiliana na changamoto za kiuchumi na kihisia.

Katika "*Seduce Me*" ya Alikiba, uanaume unajengwa kupitia mvuto wa kimapenzi, kujiamini na mamlaka ya kihisia. Mistari kama "*I'm too smart, dada*," "*they call me Kiba Rockstar*," na "*najua kupenda, nagawa mavumba*" inaonesha mwanaume anayethibitisha uwepo wake kupitia haiba, ushawishi na uwezo wa kuvutia wanawake. Hapa mwanaume anakuwa Mtendaji wa kihisia (*emotional performer)* anayepaswa kuigiza mvuto na uthabiti wa kihisia ili kuthibitisha uanaume wake. Aidha, kauli kama "*nina madinga mapya kila mmoja nampa*" zinaonesha kuwa mvuto wa mwanaume unahusishwa pia na uwezo wa kifedha na hadhi ya kijamii. Hii inaendana na Connell na Messerschmidt (2005) wanaosisitiza kuwa Uanaume tawala/uanaume wenye mamlaka ya kijamii (*hegemonic masculinity*) hujengwa kupitia mafanikio, umiliki na uwezo wa kudhihirisha nguvu mbele ya wengine. Matumizi ya Kiingereza katika wimbo huu yanaashiria athari za utandawazi katika ujenzi wa uanaume wa kisasa wa Tanzania. Kwa kutumia hoja ya Bhabha (1994), uanaume huu unaweza kueleweka kama uanaume mseto (*hybrid masculinity*) inayounganisha maadili ya jadi ya Kiafrika na taswira za kimataifa za mwanaume wa kisasa mwenye mvuto, anasa na maisha ya kidijitali. Katika nafasi ya tatu (*third space*), mwanaume wa Bongo Fleva si wa jadi kikamilifu wala wa kimagharibi kikamilifu, bali ni utambulisho mpya unaozalishwa kupitia mwingiliano wa tamaduni hizo.

Kwa upande mwingine, "*Wanaume Kama Mabinti*" ya Lady Jaydee inatoa ukosoaji wa moja kwa moja wa wanaume wanaoonekana kushindwa kutimiza matarajio ya kijamii kuhusu uanaume. Kauli kama "*wanaume kama mabinti*," "*mnalia hovyo*," na "*hamjui mnachotaka*" zinaonesha namna jamii inavyotumia lugha kudhibiti tabia za wanaume. Hapa mwanaume anayodhihirisha hisia nyingi anaonekana kuvunja kanuni za *hegemonic masculinity*. Wimbo huu unaonesha kile Connell (2005) anakieleza kama udhibiti wa kijinsia (*gender policing*), ambapo jamii huweka mipaka ya tabia zinazokubalika kwa mwanaume "halisi." Aidha, wimbo huu unaibua mvutano mkubwa wa uanaume wa kisasa: jamii inawataka wanaume wawe wa kimapenzi na wenye hisia,

lakini bado inawahukumu wanapoonekana dhaifu kihisia. Hooks (2004) anaeleza kuwa mfumo dume huwaumiza wanaume pia kwa kuwazuia kueleza hisia zao kwa uhuru.

Kwa ujumla, nyimbo hizi zinaonesha mifumo mbalimbali ya ujenzi wa uanaume katika Bongo Fleva: uanaume kama uwezo wa kiuchumi (*Mume Bwege*), uanaume kama mapambano ya maisha ya mjini (*Zali la Mentali*), uanaume kama uthibitisho wa kijamii (*Ndio Mzee*), na uanaume kama utendaji wa kihisia na starehe (*Bora Ni Enjoy* na *Seduce Me*). Wakati huo huo, *Wanaume Kama Mabinti* inaonesha namna jamii inavyoendelea kudhibiti mipaka ya uanaume kupitia ukosoaji wa kijinsia. Hivyo, Bongo Fleva inajitokeza kama nafasi ya tatu (*third space*) ya kitamaduni ambapo maana ya kuwa mwanaume huendelea kujengwa, kuvunjwa na kujengwa upya kupitia utandawazi, muziki wa kidijitali na mabadiliko ya kijamii ya Tanzania ya kisasa. Uchambuzi huu unaonesha kuwa uanaume katika Bongo Fleva si hali ya asili bali ni matokeo ya mchakato wa kijamii unaotegemea lugha, nguvu za kiuchumi, mahusiano ya kijinsia na uthibitisho wa kijamii, hivyo kufichua pia namna mfumo dume unavyounda si tu nguvu za mwanaume bali pia udhaifu wake pale anaposhindwa kufikia viwango vilivyowekwa na jamii.

### *Uanaume wa Kiuchumi, Mapenzi na Migogoro ya Mahusiano*

Muziki Bongo Fleva unaonesha kuwa ujinsishaji wa mwanaume hujengwa kupitia nguvu za kijamii zinazohusisha uchumi, mapenzi, mamlaka na hisia. Muziki huu humwonesha mwanaume kama mhusika anayepaswa kuthibitisha uanaume wake kupitia uwezo wa kifedha, uthabiti wa kihisia na mafanikio ya kimapenzi. Kwa mantiki hii, nyimbo nyingi zinaendeleza kile Connell na Messerschmidt (2005) wachokiita uanaume tawala, ambapo hadhi ya mwanaume huunganishwa moja kwa moja na uwezo wa kutoa, kulinda na kudhibiti rasilimali pamoja na mahusiano. Hivyo, kushindwa kiuchumi au kihisia hakuchukuliwi kama changamoto ya kawaida ya maisha, bali kama kupungua kwa hadhi ya uanaume wenyewe.

Katika "*Mdogomdogo*" ya Diamond Platnumz, uanaume hujengwa kama safari ya kujitafuta na kupanda kiuchumi kupitia juhudi, subira na uthabiti. Kauli kama *"nilianza mdogomdogo, leo niko juu kidogo"* zinaonesha kuwa uanaume si hali ya asili bali ni mchakato wa kujijenga kijamii na kiuchumi. Mwanaume anatambulika kupitia maendeleo yake ya kifedha na uwezo wake wa kutoka katika hali ya chini kwenda juu. Kwa mujibu wa Kimmel (2020), mwanaume wa kisasa hulazimika

kujithibitisha kila wakati kupitia mafanikio ya kijamii na kiuchumi, jambo linalofanya uanaume kuwa mradi endelevu wa ushindani na uthibitisho wa nafsi.

Mtazamo huo unaendelea katika "*Nipe Nafasi*" ya Dully Sykes ambapo mwanaume anaonekana akitafuta uhalali wa kijamii na kimapenzi kupitia uwezo wa "kuonyesha" thamani yake. Kauli *"nipe nafasi nikuoneshe mapenzi yangu"* inaonesha kuwa mwanaume hapewi uhalali moja kwa moja bali lazima ajithibitishe kupitia matendo. Hapa, mapenzi yanageuka kuwa eneo la utendaji wa kijinsia ambapo mwanaume hulazimika kuonesha uwezo wa kutoa, kupenda na kumshawishi mwanamke ili kuthibitisha uanaume wake. Hoja hii inaendana na Butler (1990) kuhusu utendaji wa kijinsia *(performativity)*, kwamba jinsia huzalishwa kupitia matendo yanayorudiwa mara kwa mara. Aidha, Hall (1997) anaonesha kuwa utambulisho hujengwa kupitia uwakilishi wa kitamaduni, hivyo "nafasi" katika wimbo huu inakuwa alama ya kukubalika kwa mwanaume ndani ya mfumo wa kijamii.

Vilevile, "*Dume Suruali*" ya Mwana FA na Vanessa Mdee inaonesha namna uanaume unavyounganishwa moja kwa moja na uwezo wa kifedha. Kauli *"dume suruali hana hela wala msimamo"* zinatumia lugha ya kejeli kuonyesha kuwa mwanaume asiye na uwezo wa kiuchumi hupoteza hadhi yake ya kijinsia. "Suruali" hapa inakuwa alama ya uanaume usio na uhalali kwa sababu hauna uchumi wala mamlaka. Hivyo, muziki huu unaendeleza fikra kwamba fedha ndiyo msingi wa mamlaka ya mwanaume katika jamii na mahusiano. Silberschmidt (2001) anaeleza kuwa mabadiliko ya kiuchumi Afrika Mashariki yamezalisha mgogoro wa uanaume kwa sababu wanaume wengi hawawezi tena kutekeleza nafasi ya jadi ya mtoa huduma. Kwa hiyo, Bongo Fleva inaakisi wasiwasi huo wa kijamii kwa kuonesha mwanaume anayepimwa kwa uwezo wake wa kifedha.

Mbali na uchumi, nyimbo hizi pia zinaonesha kuwa mapenzi ni eneo muhimu la migogoro ya kihisia na kijinsia. Katika *Sikomi* ya Diamond Platnumz, mwanaume anaonekana akiteseka kihisia lakini akishindwa kujiondoa katika mahusiano yenye maumivu. Mistari kama *"kumbe mapenzi hayataki haraka," "wivu ukanifanya nikagombana na marafiki,"* na *"ugomvi na mamangu akiniambia siambiliki"* inaonesha jinsi mapenzi yanavyogeuka kuwa chanzo cha mgogoro wa kijamii na kihisia. Hapa, mwanaume hapotezi tu utulivu wa kihisia bali pia mahusiano yake ya kijamii na kifamilia. Wivu, utegemezi wa kihisia na maumivu vinaoneshwa kama sehemu ya

uzoefu wa mwanaume wa kisasa anayepambana kati ya hisia zake binafsi na matarajio ya kijamii ya kuonekana imara.

Aidha, mstari *"moyo ukanambia Nasibu sasa mapenzi basi, ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi"* unaonesha mvutano kati ya mantiki na hisia. Mwanaume anatambua maumivu anayopitia lakini bado anaendelea kung'ang'ania mahusiano hayo. Hii inaendana na kile Waling (2019) anakieleza kama urejeleaji na uchambuzi wa hisia binafsi (*emotional reflexivity*), ambapo mwanaume ana hisia nyingi lakini hana nafasi salama ya kijamii ya kuzionesha wazi. Hivyo, uanaume katika *Sikomi* hauonekani kama uimara wa kihisia bali kama uwezo wa kuvumilia maumivu kimya kimya.

Marudio ya kauli *"sikomi"* pamoja na mistari kama *"nishafumania," "nikafumaniwa mimi,"* na *"nishagombana na watu licha ya mateso haya"* yanaonesha mwanaume aliyekwama katika mzunguko wa maumivu, usaliti na utegemezi wa kihisia. Kwa mtazamo wa Kimmel (2020), hali hii huzalisha wasiwasi wa mwanaume kuhusu kuthibitisha uanaume wake (*masculinity anxiety)*, yaani hofu ya mwanaume kupoteza hadhi yake ya kijinsia anaposhindwa kudhibiti hisia na mahusiano yake. Aidha, Ahmed (2021) anaeleza kuwa kutodhibiti uanaume kunaweza kusababisha uchumi wa hisia (*emotional economy*) inayodhibiti namna wanaume wanavyoruhusiwa kuonesha maumivu yao. Ndani ya *Sikomi*, mwanaume anaruhusiwa kuumia lakini haruhusiwi kuonekana dhaifu hadharani; badala yake analazimika kuendelea kuigiza uthabiti wa kihisia.

Kwa kutumia mtazamo wa Bhabha (1994), uanaume unaowasilishwa katika nyimbo hizi unaweza kueleweka kama uanamme mseto unaotokana na mgongano kati ya maadili ya jadi na uanaume wa kisasa. Kwa upande mmoja, mwanaume anatakiwa kuwa mwenye nguvu, mwenye uchumi na asiyeonesha udhaifu wa kihisia; lakini kwa upande mwingine, muziki wa Bongo Fleva unampa nafasi ya kueleza maumivu, wivu, utegemezi wa kihisia na kushindwa kwake katika mapenzi. Hivyo, mwanaume wa Bongo Fleva si kimya kabisa kama mwanaume wa jadi, lakini pia hajapata uhuru kamili wa kuonesha udhaifu wake bila kuhatarisha hadhi yake ya kijinsia.

Kwa ujumla, nyimbo hizi zinaonesha kuwa Bongo Fleva si burudani pekee bali ni eneo muhimu la uzalishaji wa maana za kijinsia ambapo uchumi, mapenzi na hisia hutumika kujenga na kupima uanaume. Uanaume huwasilishwa kama safari ya mafanikio ya kiuchumi, hitaji la kuthibitisha

uwezo wa kimapenzi, pamoja na uvumilivu wa maumivu ya kihisia ili kulinda hadhi ya kijamii ya mwanaume katika jamii ya Tanzania ya kisasa.

***Uanaume Mseto katika Muktadha wa Utamaduni wa Kiswahili na Athari za Utandawazi***

Sehemu hii inachunguza jinsi utamaduni wa jamii ya Kiswahili unavyoathiri ujenzi wa uanaume katika nyimbo za Bongo Fleva, hususan kupitia mabadiliko ya kijamii, utandawazi na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali. Uchambuzi unaonesha namna wasanii wanavyounda uanaume mseto (*hybrid masculinity*) unaochanganya maadili ya jadi ya Kiswahili kama heshima, wajibu wa kifamilia na mamlaka ya mwanaume, pamoja na mitindo ya kisasa inayohusisha starehe, uhuru wa kihisia, mvuto wa kimapenzi na maisha ya kidijitali. Kwa kutumia hoja za uanaume mseto na nafasi ya tatu za Homi Bhabha (1994), inaoneshwa kuwa uanaume katika Bongo Fleva si wa jadi kikamilifu wala wa kimagharibi kikamilifu, bali ni utambulisho unaozalishwa kupitia mwingiliano wa utamaduni wa Kiswahili, utandawazi na mabadiliko ya kijamii ya Tanzania ya kisasa.

Katika muktadha wa Bongo Fleva ya kisasa, uanaume hauwezi tena kueleweka kama utambulisho thabiti unaojengwa juu ya nguvu za kimwili, mamlaka ya kifamilia na ukimya wa kihisia pekee, bali kama mchakato wa kijamii unaobadilika kulingana na mazingira ya kiutamaduni, kiuchumi na kiteknolojia. Ndani ya mazingira haya, uanaume mseto unaeleza namna wanaume wanavyochanganya vipengele vya uanaume wa jadi na vya kisasa vinavyoruhusu udhihirisho wa hisia, udhaifu na utegemezi wa kihisia. Kwa mujibu wa Connell na Messerschmidt (2005), uanaume tawala hujengwa juu ya mamlaka, uwezo wa kiuchumi na udhibiti wa kihisia, lakini katika Bongo Fleva ya kisasa mfumo huu unaingia katika mvutano kutokana na athari za utandawazi na mabadiliko ya kijamii. Anderson (2021) anaeleza kuwa hali hii husababisha kile kinachojulikana kama mgogoro wa uanaume (*masculinity crisis*), ambapo matarajio ya jadi hayaendani tena kikamilifu na uhalisia wa maisha ya kisasa.

Katika *Sikomi* ya Diamond Platnumz, uanaume unaoneshwa kupitia maumivu ya mapenzi, majuto na utegemezi wa kihisia unaokiuka taswira ya jadi ya mwanaume mtawala. Mistari kama: *"Wanasemaga mapenzi safari, unavyopita ndo jinsi unajongea…"* na *"Mwenzenu nikaoza haswa, na kujitia kitandani mjuzi"* inaonesha mwanaume anayekubali udhaifu na kushindwa kimapenzi

hadharani. Hapa, uanaume unajengwa kama utendaji wa kijinsia wa Butler (1990), ambapo maana ya kuwa mwanaume hutengenezwa kupitia matendo na lugha, si asili ya kudumu. Aidha, kauli kama *"Moyo ukanambia Nasibu sasa mapenzi basi, ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi"* inaweka uanaume ndani ya nafasi ya tatu ya Bhabha (1994), ambapo mgongano kati ya uthabiti wa jadi na uwazi wa kihisia wa kisasa huzalisha utambulisho wa mseto. Hooks (2004) anaongeza kuwa mfumo dume huwafundisha wanaume kuamini kuwa utoaji wa mali ni njia ya kupata mamlaka katika mahusiano, hali inayoonekana pia katika kauli ya: *"Nilimuhongaga gari aliponambia ana mimba…"*.

Katika *Wanaume Kama Mabinti* ya Lady Jaydee, uanaume unakosolewa kupitia lugha ya kudhalilisha wanaume wanaoshindwa kutimiza matarajio ya kijamii. Kauli kama *"Wanaume kama mabinti"* na *"mnalia hovyo"* zinaonesha namna jamii inavyotumia lugha kama chombo cha udhibiti wa kijinsia (*gender policing*), ambapo mipaka ya uanaume "halisi" huwekwa na kulindwa. Kwa mujibu wa Kimmel (2020), uanaume mara nyingi hujengwa juu ya hofu ya "kutokuonekana mwanaume vya kutosha," hivyo ukosoaji huu unaimarisha viwango vya mfumo dume. Waling (2019) anaeleza kuwa wanaume wanaokosa uwezo wa kiuchumi hupoteza mtaji wa uanaume (*masculine capital*), hali inayoleta mgogoro wa utambulisho. Hivyo, wimbo huu hauwalengi wanaume binafsi pekee bali unaonesha jinsi jamii inavyodhibiti maana za uanaume kupitia lugha na utamaduni.

Katika *Dume Suruali* ya Mwana FA na Vanessa Mdee, uanaume unawekwa katika mvutano kati ya fedha, mapenzi na mamlaka ya kijinsia. Kauli kama *"We ni dume suruali kaa mbali nami"* na *"Jambo la kimapenzi tusileteane ujambazi"* zinaonesha mapenzi kama eneo la majadiliano ya nguvu na uchumi wa kihisia. Connell na Messerschmidt (2005) wanaeleza kuwa uanaume tawala hujengwa juu ya udhibiti wa uchumi na mahusiano, lakini hapa mwanamke anaonekana kuwa na uwezo wa kukataa na kujadiliana, hivyo kuyumbisha mfumo huo. Illouz (2023) anaeleza kuwa mapenzi katika jamii ya kisasa yamefungamanishwa na mantiki ya soko, ambapo hisia na mahusiano huathiriwa na mtaji wa kijamii na kiuchumi. Vilevile, Gill (2022) anaonesha kuwa utamaduni wa kidijitali umeongeza uwepo wa wanawake wenye sauti katika kuhoji mahusiano ya kijinsia.

Kwa ujumla, nyimbo hizi zinaonesha kuwa uanaume katika Bongo Fleva ni eneo la mvutano na mazungumzo endelevu ya kijinsia. Wanaume wanaonekana kuishi ndani ya hali ya mpito ambapo wanapaswa kuwa wenye nguvu lakini pia wenye hisia; watawala lakini pia washirikiano; wenye mamlaka lakini pia wanaoathirika kihisia. Elliott (2022) anaeleza kuwa utamaduni wa kidijitali umeufanya uanaume kuwa *utendaji wa kijinsia* unaoonyeshwa hadharani kupitia mafanikio, hisia na mahusiano. Hivyo, *uanaume mseto* katika Bongo Fleva hauwakilishi kuanguka kwa mfumo dume, bali marekebisho yake ndani ya mazingira mapya ya kijamii, kiuchumi na kidijitali. Kwa mantiki hii, "kuwa mwanaume" katika Bongo Fleva ni mchakato endelevu wa kujenga, kuvunja na kujenga upya utambulisho ndani ya nafasi ya tatu ambapo mila, mfumo dume na usasa vinaendelea kugongana na kuzalisha maana mpya za uanaume.

**Hitimisho**

Kwa jumla, uchunguzi huu unaonesha kwamba Bongo Fleva haipaswi kusomwa kama sanaa ya burudani pekee, bali kama uwanja wa kijamii unaozalisha, kuimarisha na wakati huo huo kupinga maana za uanaume. Kwa upande mmoja, nyimbo zilizochambuliwa zinaendelea kuhalalisha mfumo dume kwa kumjenga mwanaume kama mtoa riziki, mwenye mamlaka ya kijamii, nguvu ya kifedha na uthabiti wa kihisia. Hapa, uanaume unaendelea kupimwa kwa uwezo wa kiuchumi, umaarufu na uwezo wa kudhibiti mahusiano ya kijinsia, jambo linaloendana na hoja ya Connell (2005) kuhusu uanaume tawala kama mfumo unaodumisha uongozi wa mwanaume katika jamii.

Hata hivyo, kwa upande mwingine, nyimbo hizo hizo zinapindua taswira hiyo kwa kuonesha mwanaume akiwa katika hali ya udhaifu wa kihisia, maumivu ya mapenzi, usaliti na kushindwa kukabiliana na shinikizo za kijamii. Hapa, mwanaume anaonekana kulia kimya kimya, kujificha nyuma ya ulevi, au kukiri uchovu wa kihisia. Hali hii inaendana na hoja ya Hooks (2004) kwamba mfumo dume haumdhuru mwanamke pekee bali pia humuumba mwanaume katika mfumo wa ukandamizaji wa kihisia unaomkataza kuonyesha udhaifu. Kwa hiyo, uanaume katika Bongo Fleva unakuwa kinyume cha picha moja thabiti; ni utambulisho unaojigawa kati ya nguvu na kuvunjika.

Kutokana na mvutano huu, uanaume unaojitokeza katika muziki huu unaweza kueleweka vizuri kama eneo la mapambano ya kiitikadi kati ya uanaume wa jadi na uanaume wa kisasa. Pia ni sehemu ya ukinzani kwa sababu mwanaume huyo huyo anatakiwa kuwa imara na wakati huohuo

anaruhusiwa kuumia; anatakiwa kutawala kihisia lakini pia anatarajiwa kuwa mnyenyekevu na mwenye hisia. Zaidi ya hapo, ni sehemu ya majadiliano na upatanishi hasa pale ambapo maana ya uanaume haikamilishwi na mfumo mmoja, bali hujengwa upya kupitia mwingiliano wa utamaduni wa jadi, utandawazi, mitandao ya kijamii na mabadiliko ya kiuchumi.

Kwa kutumia mtazamo wa Judith Butler (1990), hali hii inaonesha kuwa uanaume si utambulisho wa asili bali ni utendaji unaorudiwarudiwa (*gender performativity*) unaobadilika kulingana na mazingira ya kijamii. Vilevile, Walby anaeleza mfumo dume kama mfumo unaojirekebisha na kuendelea kubadilika badala ya kubomoka moja kwa moja, jambo linaloonekana wazi katika Bongo Fleva ambapo mfumo dume unaendelea kuwepo lakini kwa sura mpya ya kihisia na kisasa. Kwa upande wake, Ratele (2020) anaonya kuwa uanaume wa Kiafrika hauwezi kueleweka nje ya muktadha wa kihistoria na kiuchumi, ambapo shinikizo la kuwa “mwanaume kamili” linatokana na vikwazo vya kijamii na kiuchumi vinavyobadilika kila wakati.

Hivyo basi, hitimisho kuu la uchambuzi huu ni kwamba Bongo Fleva inazalisha uanaume unaoishi katika mvutano wa kudumu: uanaume unaojengwa na kuvunjwa kwa wakati mmoja. Ni uanaume unaothibitisha nguvu lakini pia unakiri udhaifu; unaodumisha patriarchy lakini pia unauhoji; unaoonyesha mamlaka lakini pia unafichua maumivu. Kwa mantiki hii, uanaume katika Bongo Fleva ni zaidi ya utambulisho ni mchakato wa kijamii unaoendelea, unaogongana na unaojadiliwa kila mara ndani ya nafasi ya muziki kama eneo la uzalishaji wa maana za kijinsia.

## Marejeleo


Adichie, C. N. (2013). *Americanah*. Nigeria: Alfred A. Knopf.

Adichie, C. N. (2014). *We should all be feminists*. Fourth Estate. Babalola, E. (2023). African hip hop, identity, and youth politics. *Journal of African Cultural Studies*. https://doi.org/10.1080/13696815.2023. Ilisomwa tarehe 9 Mei 2026

Ahmed, S. (2021). *The cultural politics of emotion* (2nd ed.). Edinburgh: Edinburgh University Press.

Alex Perullo. (2011). *Live from Dar es Salaam: Popular music and Tanzania's music economy*. Bloomington: Indiana University Press.

Ambler, C. (2021). Emotional authority and patriarchy in African popular culture. *African Studies Review, 64*(4), 112–130. https://doi.org/10.1017/asr.2021.45. Ilisomwa tarehe 20 Mei 2026.

Babalola, S. (2023). Masculinity and men's challenges in contemporary African societies. *African Journal of Social Work,* 15 (2), 21-30.

Berg, B. L. (2009). *Qualitative research methods for the social sciences*. Pearson. https://www.pearson.com/en-us/subject-catalog/p/qualitative-research-methods-for-the-social-sciences/P200000003295. Ilisomwa tarehe20 Mei 2026

Beukes, L. (2013). *The shining girls*. UK: Mulholland Books.

Bhabha, H. K. (1994). *The location of culture*. London: Routledge.

Bjarnesen, J., et al. (2023). Masculinities and social change in Africa. *African Affairs*. https://doi.org/10.1093/afraf/adad0xx. Ilisomwa tarehe 15 Mei 2026.

Braun, V., & Clarke, V. (2006). Using thematic analysis in psychology. *Qualitative Research in Psychology*. https://doi.org/10.1191/1478088706qp063oa. Ilisomwa tarehe 27 Mei 2026

Bulawayo, N. (2013). *We need new names*. New York: Reagan Arthur Books.

Butler, J. (1990). *Gender trouble: Feminism and the subversion of identity*. London: Routledge.

Canclini, N. G. (1995). *Hybrid cultures: Strategies for entering and leaving modernity*. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Caywood, K., & Darmstadt, G. L. (2024). Engendering health systems and gender-inclusive approaches in global health. *Global Public Health, 19*(2), 145–160. https://doi.org/10.1080/17441692.2024.0000000. Ilisomwa tarehe15 Mei 2026

Chung, H. (2017). Gender, identity and social inequality in contemporary societies. *Gender Studies Journal*, *12*(1), 33–49.

Clowes, L. (2020). Men and masculinities in Africa: New directions in gender studies. *African Studies Review, 63*(4), 1–15. https://doi.org/10.1017/asr.2020.45. Ilisomwa tarehe 15 Mei 2026.

Connell, R. W., & Messerschmidt, J. W. (2005). Hegemonic masculinity: Rethinking the concept. *Gender & Society*, 19(6), 829–859

Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches*. *Gender & Society, 19*(6), 829–859. https://doi.org/10.1177/0891243205278639. Ilisomwa tarehe 15 Mei 2026.

Connell, R. W. (1995). *Masculinities*. Berkeley, CA: University of California Press.

Connell, R. W. (2005). *Masculinities* (2nd ed.). Berkeley: University of California Press. https://www.ucpress.edu/book/9780520254018/masculinities. Ilisomwa tarehe 25 Aprili 2026.

Dankoor, K., Stephens, R., & van den Bogaert, S. (2023). Rap music and masculinity formation. *Journal of Youth Studies*. https://doi.org/10.1080/13676261.2023. Sage.

Dankoor, K., Stephens, D., & ter Bogt, T. (2023). *Drip too hard? Commercial rap music and perceived masculinity ideals and actual self-evaluations among Black U.S. and Dutch adolescent men*. *Sexuality & Culture, 27*(1), 57–77. https://doi.org/10.1007/s12119-022-10003-9. Ilisomwa tarehe 14 Aprili 2026.

Denzin, N. K. (1978). *The research act: A theoretical introduction to sociological methods*. Columbus: McGraw-Hill.

Elliott, K. (2022). Digital masculinity and the performance of self in social media culture. *New Media & Society, 24*(5), 1201–1218. https://doi.org/10.1177/14614448211017845. Ilisomwa tarehe 28 Machi 2026.

Ezeugwu, C. R., & Ojedokun, O. (2020). Masculine norms and mental health of African men. *Heliyon, 6*(12), e05650.https://doi.org/10.1016/j.heliyon.2020.e05650. Ilisomwa tarehe 20 Machi 2026.

Gill, R. (2009). Beyond the "sexualization of culture" thesis: An intersectional analysis of "sixpacks," "midriffs" and "hot lesbians" in advertising. *Sexualities, 12*(2), 137–160.

Grabe, S. (2015). *Women's empowerment and global health: A twenty-first-century agenda*. Berkeley:  University of California Press.

Hall, S. (1996). *Cultural identity and diaspora*. In J. Rutherford (Ed.), *Identity: Community, culture, difference* (pp. 222–237). Lawrence & Wishart.Hooks, b. (2004). *The will to change: Men, masculinity, and love*. New York: Washington Square Press.

Hooks, B.(2000). *Feminism is for everybody: Passionate politics*. Boston:  South End Press.

John, Y. M. (2025). Reversed gender roles of women in Bongo Flava songs: A critical examination. *East African Journal of Arts and Social Sciences, 8*(3), 688–699. https://doi.org/10.37284/eajass.8.3.3786. Ilisomwa tarehe 12 Aprili 2026.

John, P. (2025). Engendering and social justice in East African communities. *Journal of African Social Studies, 14*(1), 44–60.

John, P., & Kilatu, R. (2025). Gender inclusion and social transformation in Tanzania. *East African Journal of Arts and Social Sciences, 8*(2), 88–103.

John, Y. M. (2025). *Reversed gender roles of women in Bongo Flava songs*. *East African Journal of Arts and Social Sciences, 8*(1), 45–58.

Uma A. (2024). Youth culture, music and moral values in contemporary Tanzania. *Tanzania Journal of Cultural Studies, 6*(1), 55–73.

Katambi, S. (2021). Representation of gender in contemporary Bongo Fleva music. *Journal of Kiswahili and African Studies, 3*(2), 67–84.

Khamis, S. (2020). *The representation of women and patriarchal ideology in Bongo Flava music in Tanzania* (Master's dissertation, University of Dar es Salaam).

Kimmel, M. (2017). *Angry white men*. New York: Nation Books.

Kimmel, M. (2020). *Angry white men* (Rev. ed.). Bold Type Books. https://boldtypebooks.com/titles/michael-kimmel/angry-white-men/9781568589642/

Kimmel, M. (2020). *Angry white men: American masculinity at the end of an era* (Rev. ed.). New York: Bold Type Books.

Krippendorff, K. (2018). *Content analysis: An introduction to its methodology*. Sage. https://us.sagepub.com/en-us/nam/content-analysis/book258450. Ilisomwa tarehe 27 Mei 2026

Kupers, T. A. (2005). Toxic masculinity as a barrier to mental health treatment in prison. *Journal of Clinical Psychology, 61*(6), 713–724.

Kweka, H. (2013). Lugha na utambulisho wa kijinsia katika muziki wa Bongo Fleva. *Mulika, 32*(1), 78–95.

Lawson, D., Dubin, A., & Mwambene, L. (2019). *Ensuring African women's access to justice: Engendering rights for poverty reduction in Sub-Saharan Africa*. Uppsala: Nordic Africa Institute.

Lawson, D., Dubin, A., & Mwambene, L. (Eds.). (2020). *Gender, poverty and access to justice: Policy implementation in Sub-Saharan Africa*. Routledge. https://doi.org/10.4324/9780429280385. Ilisomwa tarehe 27 Mei 2026

Lawson, D., Dubin, R., & Mwambene, L. (2019). Gender justice in Sub-Saharan Africa. *African Human Rights Law Journal*. https://journals.assaf.org.za/index.php/ahr

Limbe, A. (2024). The portrayal of empowered women in contemporary Bongo Flava music. *Mulika Journal of the Institute of Kiswahili Studies, 43*(2), 112–128.

Mama, A. (2011). Feminism and gender studies in Africa. *African Gender Institute Working Papers*. https://agi.ac.za. Ilisomwa tarehe 23 Machi 2026.

Mama, A. (2011). What does it mean to do feminist research in African contexts? *Feminist Review, 98*(1), 4–20. https://doi.org/10.1057/fr.2011.22. Ilisomwa tarehe 22 Mei 2026.

Mhando, J. (2020). *Uanaume na changamoto za vijana wa kiume katika jamii ya Tanzania ya kisasa*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlaga, J. (2017). Gender discourse and engendering processes. *Tanzania Journal of Development Studies*. https://www.tjds.or.tz. Ilisomwa tarehe 22 Mei 2026.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi karne ya 21*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mnenuka, A. (2010). Uwakilishi wa mwanamke katika nyimbo za Bongo Fleva. *Kioo cha Lugha, 8*(1), 102–118.

Mnisi, R., & Thete, I. P. (2025). Internalised struggles faced by boys and men: An analysis of Matalane Mokgatla’s song “Men Speak Out.” *International Journal of African Renaissance Studies, 20*(2), 81–100. https://doi.org/10.1080/18186874.2025.2577332. Retrieved on 22 May 2026.

Mtallo, G. R., & Msoffe, M. J. (2025). An assessment of language choice in contemporary Tanzanian music. *Business Education Journal, 4*(1), 1–15. https://doi.org/10.54156/wdmt5n43. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2026.

Mulvey, L. (1975). Visual pleasure and narrative cinema. *Screen, 16*(3), 6–18.

Mwakibete, E. A. (2022). Masculinity in Tanzanian Bongo Fleva: Dume Suruali analysis. *Journal of East African Studies*. https://doi.org/10.1080/17531055.2022. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2026.

Mwakibete, E. A. (2022). Tanzanian popular songs disapprove modern harmful masculinities: Analysing Mwana FA's song "Dume Suruali." *Tanzania Journal of Sociology, 8*(1), 154–175.

Nnaemeka, O. (1998). *Sisterhood, feminisms and power: From Africa to the diaspora*. Trenton, NJ: Africa World Press.

Our Watch. (2018). *Challenging gender stereotypes and preventing violence: Evidence review*. Melbourne: Our Watch.

Patton, M. Q. (2015). *Qualitative research and evaluation methods*. Sage.

Penina Mlama. (1991). *Culture and development: The popular theatre approach in Africa*. Uppsala: Scandinavian Institute of African Studies.

Perullo, A. (2005). *Hooligans and heroes: Youth identity and hip-hop in Dar es Salaam, Tanzania*. *Africa Today, 51*(4), 75–101.

Perullo, A. (2011). *Live from Dar es Salaam: Popular music and Tanzania's music economy*. , Bloomington:  Indiana University Press.

Pierson, M. (2021). From rage to riches: Swag and capital in the Tanzanian hip hop industry. *Popular Music, 40*(1), 74–92.

Rao, A. (2014). Gender equality and engendering development processes. *Gender & Development, 22*(1), 1–17. https://doi.org/10.1080/13552074.2014.889339. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2026..

Ratele, K. (2013). Masculinities without tradition. *Politikon, 40*(1), 133–156.

Ratele, K. (2020). *The world looks like this from here: Thoughts on African psychology*. Johannesburg: Wits University Press.

Rens, S. E. (2023). Afrobeats and gender representation. *Popular Music and Society*. https://doi.org/10.1080/03007766.2023. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2026..

Saimon, M. (2019). Co-constructing or deconstructing gender identity? A multimodal critical discourse analysis of Bongo Flava song video *Niambie*. *Profetik: Jurnal Komunikasi, 12*(1), 5–20

Silberschmidt, M. (2001). Disempowerment of men in rural and urban East Africa: Implications for male identity and sexual behavior. *World Development, 29*(4), 657–671

Stuart Hall. (1997). *Representation: Cultural representations and signifying practices*. Sage Publications.

Suriano, M. (2007). *Mzungu Kichaa and the rise of Bongo Flava music in Tanzania*. *Journal of African Cultural Studies*, *19*(2), 207–222.

Suriano, M. (2021). Hip-hop and Bongo Flava music in contemporary Tanzania: Youths' experiences, agency, aspirations and contradictions. *Africa Development*, *46*(1), 89–110. https://doi.org/10.57054/ad.v46i1.1234. Ilisomwa tarehe 15 Machi 2026..

Suriano, M. (2021). Youth culture and Bongo Fleva. *Swahili Forum*. https://www.jstor.org/stable/

Talakinu, R. (2023). Engendering social inclusion in African cultural contexts. *African Sociological Review*, *27*(2), 91–108.

Tamale, S. (2020). *Decolonization and Afro-feminism*. Canada: Daraja Press.

Tatamentan, D. N. (2026). The silent burden: Exploring men's mental health in Cameroon amidst societal pressures and responsibilities. *ShodhSamajik: Journal of Social Studies*, *3*(1), 1–15.

Thomas, P., & Bulaya, K. (2024). *Utandawazi na mabadiliko ya maadili katika muziki wa Bongo Fleva Tanzania*. *Jarida la Kiswahili*, *87*(1), 76–91.

Waling, A. (2019). Rethinking masculinity studies. *Journal of Men's Studies, 27*(1), 89–107. https://doi.org/10.1177/1060826518818059. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2026.